

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



Unapojibu tafadhali taja  
Kumb. Na. MDC/S.20/VOL.V/5/166

16/04/2021

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo;-

**1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III – NAFASI 2**

**1.1 Sifa za Mwombaji:-**

1. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne/Sita
2. Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo:
  - Utawala
  - Rasilimali watu
  - Sheria
  - Maendeleo ya Jamii
  - Elimu ya Jamii
  - Usimamizi wa Fedha au
  - Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.2 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Viwango vya Serikali kwa ngazi ya Mshahara **TGS B** kwa Mwezi

**1.3 MAJUKUMU YA KAZI**

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezai wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kuratibu Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji

#### 1.4 MASHARTI YA JUMLA

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na Umri wa Miaka 18 hadi 45
- “Testimonials, Provisional Results, Statement of Result” na hati za matokeo kidato cha Nne na Sita (form IV na VI Result Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliosoma Nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- Uwasilishaji taarifa za sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua Stahiki za Kisheria
- Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano

#### 1.5 NAMNA YA KUTUMA MAOMBI; -

Kila muombaji wa kazi awasilishe barua iliyoandikwa kwa mkono ikiambatana na;-

- Wasifu Binafsi (CV)
- Vivuli vya Vyeti vya Elimu na Ujuzi
- Majina matatu ya wadhamini
- Cheti cha kuzaliwa
- Picha mbili za “Passport Size”

1.6. Maombi yote yatumwe kupitia anuani ya posta kama ifuatavyo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 237,

**RUJEWANA – MBARALI.**

1.7 Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/04/2021 Siku ya Ijumaa, muda wa 9.30 alasiri



Kivuma H. Msangi,  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
**MBARALI.**